Kwa kubaki bomani mwa masomo

# Kila mwanafunzi apashwa kulipa Zaïre 3.672

### *Minerval ni zaïre 20 kwa mwaka

Habari zinazoaminika kutoka Nyofu, zaeleza kuwa prezidenti wa chama jimboni aliye pia liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Mwando Nsimba amechukua mnamo tarehe 26 agusti iliyopita, hatua ya kupanga daftari ya malipo mbali mbali katika masomo ya msinji na yale ya sekondari popote jimboni. Hatua hiyo itaanzishwa mnamo siku za usoni hasa zaidi wakati masomo yatakapofunguliwa.

Kufuatana na hatua hiyo, "minerval" ilipangwa kwa zaïre 20 kwa malipo ya kila mwanafunzi kwa mwaka mmoja. Shirika linalohusika na ukingo wa watu na mali zao (SONAS) litapewa zaïre 10 na kila mwanafunzi kwa mwaka mmoja na muungano wa wazazi (ANAPEZA) utatolewa zaïre 5 na kila mwanafunzi kwa mwaka mmoja. Malipo mengine yalipangwa namna ifuatayo :

-Masomo ya msinji: zaïre 30 kwa mwaka kila mwanafunzi

-Masomo ya sekondari (pédagogique et littéraire): zaïre 50 kwa mwaka kila mwanafunzi

-Ujuzi wa viwanda (technique industrielle):zaïre 1.500 kila mwanafunzi kwa mwaka

-Ujamii (social) :zaïre 100 kila mwanafunzi kwa mwaka

-Mlimo na ufugaji wanyama: zaïre 300, kwa mwaka kila mwanafunzi

-Uchumi (commercial): zaïre 150 kila mwanafunzi kwa mwaka

-Ujuzi wa magari: zaïre 350 kwa mwaka, kila mwanafunzi

-Userumala na ujenzi wa nyumba: zaïre 150 kwa mwaka kila mwanafunzi.

Kusudi ya kubaki katika boma la masomo (internat), kila mwanafunzi aazimishwa kuchungua kwa karibu utumizi wa feza hizo kusudi wanafunzi wanaobaki bomani mwa masomo (internes) wapewe chakula kizuri na waishi bila matatizo yoyote.

Liwali Mwando aliwakokota pia masikio wale wote wasiopenda kusikia mashauri ya viongozi wa Chama na ambao wanayo zoezi ya kutafuta kwa njia zote namna ya kuwina nyuma ya migongo ya wakaaji. Wawe hakika kuwa watajionea "cha mtema kuni".

**Kaboyi Habimana.**

Kinshasa

# Watu 12 walifariki kutokana na msiba ya ndege

Siku ya posho tarehe 24 Ogusti iliyopita, ndege moja ndogo (petit porteur) iliyokuwa ikitoka kwenyi uwanja wa ndege wa Ndolo na kujielekeza Boma ilianguka katika mkoa wa Matonge na kusababisha vifo vya watu 9 kwa rafla. Wengine watatu walifariki punde kidogo tu kisha kupelekwa kunako hospitali Mama Yemo huko Kinshasa. Wale waliojeruhiwa wapatikana katika hali mbaya wakipata matibabu ya madaktari. Mmoja kati ya mashahidi wa msiba huo, mwananchi, ...OMBELE, aliyeulizwa na wapashaji habari wa OZRT alieleza kuwa alikuwa mlangoni mwa nyumba yake. Mara akaona ndege hiyo ikishuka vibaya na kukwaruza mlangoni mwa

kukwaruza miti na nyumba. Alipotambua hali hiyo, akashikwa na woga na kisha akakimbilia nyumbani. Kisha kidogo akasikia shindo kubwa wakati ndege hiyo ilipojitwanga chini. Moto mkali ukawaka na kuwateketeza wazungu watatu waliokuwamo. Kati ya marehemu hao wazungu mulikuwa mtaliana mmoja, mswisi mmoja na mzaliwa - Osçriani (Autriche) mmoja.

Aliporudi nyumbani kutoka katika ziara iliyompeleka Sénégal na Togo, raïs Mobutu na mkewe, akina mama Bobi Ladawa walijielekeza hima nafasi msiba huo ulitendeka mbele ya kwenda kuwatizama wale walio bado hospitalini. Kwa kuomboleza jamaa ya wale waliofariki, mareshali Mobutu alibaki nao muda wa siku nzima na akamuomba mganga wa hospitali Mama Yembo amtolee daftari ya madawa inayohitajika kwa kuokoa maisha ya wale wanao tibabiwa bado hospitalini.

Ulimwenguni kote watu waanza kushikwa na woga siku hizi kutokana na ajali za ndege. Kwani siku si nyingi, watu 350 waliteketea nchini Ujapani, hapo majuzi ilikuwa zamu ya wengine 58 walioaga dunia huko London, mji mkuu wa ufalme wa Uingereza. Watu waanza sasa kujiuliza kuwa ni jambo gani linalowafikia wasafiri wa njia ya anga.

**Lubunga K'Yoba.**

## Je umesikia...?

**KAMA uwizi wa vyombo vya moto wa stimu wazidishwa mjini Bukavu ? Hasa ule wa vibweta vya kupima moto huo. Kwani kibweta (coffret) kimoja chauzishwa zaïre 4.000 kwa pigo mjini Bukavu.**

**Uwizi huo watukia, kwani shirika SNEL laonekana kushindwa na kazi mjini Bukavu kwa upekee na jimboni mwa Kivu kwa jumla. Shirika hilo hulazimisha wanunuzi (clients) wake eti yeyote anayehitaji moto wa stimu nyumbani na penginepo walazimishwa kununua kibweta, singa na vifaa vyote vya lazima. Ingawa vyote vilipashwa kutolewa na shirika hilo. Na bila kusahau lwa...**

**Si hiyo ndio mungwana hujisema : Bora kidogo kwa haki kuliko mali nyingi kwa uovu na mla mbuzi hulipa ngombe.**


# JUA

## *Gazeti la Kivu*

**Mwaka wa 12 n° 283 Tarehe 7 mpaka 13 Septemba 1985**

**Kiongozi : Mutiri-wa-Bashara**


# Hatari mlangoni : Kumbe tembo wateketezwa !

### *Pembe 530 zilishikwa huko Sake

Mungwana husema: Siku za mwizi ni arubaini. Kweli masemi hayo hayo si ya uwongo kwani habari zinazoaminika na zilizotolewa na mwandishi wetu Wakilongo Nyembo ambaye ahusika na kituo chetu mjini Goma zajulisha kuwa pembe za tembo yapata 530 zilishikwa kunako barabara toka Kanyabayonga hadi Sake, katika mtaa wa Masisi. Pembe hizo zilikuwa zikisafirishwa kimagendo na bwa Kaba Souleymane, mzaliwa-Guinea.

Zimeshikwa je ? Pembe hizo zilionekana baada ya msiba wa gari ambamo zilikuwa zikisafirishwa kwa kupelekwa katika nchi jirani. Na huko, wasema, duka kazaa zimetwikwa na kuendesha uchuuzi kimagendo wa viashara hivyo. Kisha msiba huo, pembe 530 zilishikwa palepale, zingine 30 zilipatikana kwenye makao ya wakaaji. Kulingana na idadi hiyo, yaonekana wazi kuwa tembo 300 zilisagwa bila huruma katika shamba la wanyama jimboni mwa Kivu na Zaïre ya Juu. Bwana Souleymane alikuwa akitokea mjini Kisangani ambako aishi tangu mwaka wa 1978.

Aliposambishwa, mgeni huyo mjanja alijibu kwa maulizo ya waamzi kunako Korti kuu la mji wa Goma yakuwa na Wana-Zaïre ndio walimuunga mkono na hawezi kutoa vitambulisho vyao.

Hum ! Kwa kweli baada ya kitendo hicho, sasa tupo hakika kama viongozi kazaa na wananchi wenyi vyeo vikuu serikalini na chamani ndio waunga mkono wauaji wa wanyama porini.

Sikieni mambo. Baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 8 na kulipa Serikali kiasi cha Zaïre milioni 26, mwana-Guinea Souleymane asema kisirisiri na bila vipenge kwa marafiki na watu fulanifulani kama hana uwasiwasi wowote kwani yupo hakika kama haiwezekane kamwe afanye hata mwezi moja katika jela la mji wa Goma.

Kusudi pembe hizo, zisipelekwe mahali pasipojulikana, ziliweza kuchungwa na mwananchi Ngezayo Safari, mmoja kati ya viongozi wa Shirika linalohusika na kazi wa ardhi na utalii katika shamba la wanyama (IZCN) baada ya pembe hizo kusafirishwa na kupimwa uzito mjini Goma. Pia safarini mwake mjini Goma, kiongozi mkuu wa shirika hilo la IZCN aliweza kuchungua kwa karibu namna gani ya kusafirisha pembe hizo toka Goma hadi mjini Kinshasa.

Tutawakumbusha wasomaji wetu ya kuwa uchuuzi na usafirishaji kimagendo wa pembe za tembo wazidishwa siku kwa siku kwani mbele ya hapo pembe zingine 76 zilishikwa kwenye mipaka ya Rwanda na Zaïre hapo mjini Gisenyi. Na wakati Prezidenti wa Chama na liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Mwando Nsimba aliwapokea katika masimulizi rasmi waandishi wa habari waliokuwa wakimsindikiza safarini mwake katika mitaa ya Walikale na Masisi, mheshimiwa huyo alinena kuwa mwindaji mkubwa wa nyama za pori kimagendo ni kiongozi wa kazi za Chama-serikali. Kwani ni wao wanaopana njia rahisi kwa uwingo wa wanyama hao kama vile tembo, na kazalika.

Basi kutokana na kitendo hicho tulichokitaja hapo juu, pahali pa kumhukumu mtenda maovu Souleymane kifungo cha miaka 8 na malipo ya pesa nyingi ambazo labda hawezi kupata, yafaa aazibiwe vikali akitiwa kwenyi mlingoti, ATUNGIKWE, ASULUBIWE kama tembo zile na afe. Ni hatari kabisa tembo zinazoshambuliwa na waharama namna hao bila huruma zitamalizika kama viongozi na wakuu nchini hawachukuwe mipango muhimu ya kukinga wanyama hao.

**Bisimwa L-B. Tserou**